

Wareno watashtakiwa vikubwa zaidi ya kosa hili

Nguzumbe

April 13/67

KESI ya Wareno wale wawili waliongia Tanganyika bila ya sheria iliendelea tena juzi asubuhi mbele ya Magistrate wa Dar es Salaam, Bwana L. Duff. Hii ilikuwa mara ya nne na watu walijaa kusikiliza wengine wakichungulia madirishani.

Mkalimani hakupatikana na ikabidi kungoja kwa dakika thelathini hadi Assistant Superintendent wa Polisi, Bwana M.L. Baraganza kuwasili toka kazini mwake.

Akiongoza mashtaka, Bw. Chitepo aliiomba korti kuahirisha tena kesi hiyo kwa vile polisi walikuwa bado kumaliza kupeleleza zaidi juu ya kesi hiyo toka nje ya Tanganyika.

Matakwa ya watu

"Kama ninavyohusika kufuata mapendekezo ya Serkali," alisema Bw. Chitepo, "nakuomba mheshimiwa washtakiwa warudishwe tena rumande, ingawa wamekaa kwa muda mrefu hakuna njia ya kuwatolea dhama kwa vile wao si watu wa Tanganyika."

Tangu walipofikishwa kortini kwa mara ya

mwisho, Serkali ilitaka upelelezi ufanywe zaidi kutoka nchi nje ya Tanganyika, na kwa bahati mbaya hatua hiyo haijakamilika. Kesi hii ya kuingia nchini ni chanzo tu, cha mashtaka makubwa zaidi yatakayofuata.

"Si nia yetu kuwaweka katika rumande kwa muda mrefu isipokuwa ya kuendesha upelelezi zaidi wa makosa yao."

Magistrate aliwaeleza washtakiwa hao juu ya kuahirishwa kwa kesi, kuwekwa rumande, kuendelezwa kwa upelelezi na juu ya mashtaka makubwa mengine na akawa uliza

iwapo walikuwa na la kusema.

Mshtakiwa wa kwanza, Jacinto Soares Veloso alisema kuwa alipenda kueleza kisa kilichowafanya waje Tanganyika. "Nilitaka kuingia chama cha upinzani kwa utawala Dr. Salazar."

"Baada ya kusaidia wa tu wa Mozambiki nisingekaa Tanganyika bali ningekwenda mahali pengine. Siwezi kurudi Ureno ama katika makoloni yake kwa vile askari polisi wa siasa na wa siri wangenikamata na kunifanya mabaya. Kwa sababu hiyo tulikuja hapa."

Sina la kusema

Hapo Magistrate alimkatisha Veloso kuwa ha

Inaendelea uk.

kutaka eleze sababu yakuja Tanganyika ama kuwa kinyume na Salazar na chama chake. "Ninachotaka useme ni juu ya mamombi ya Mwongoza Mashstaka na kama unataka nikufanyie nini." (4)

"Una lolote la kusema juu ya ombi la Mshtaka?" aliuliza Bw. Hakimu. Veloso alijibu kuwa hakuwa na la kusema. "Hujali kurudi tena rumande?" Bwana Hakimu aliuliza tena. "Sina la kusema," alijibu tena.

Mshtakiwa wa pili, Joao dos Santos Ferreira alisema kuwa wakika hawakujua namna korti inavyoendeshwa kwa vile ilikuwa awali kufika kortini. Juu ya rumande alisema kuwa wataendelea kukaa ruma nde.

Korti haipendi (5)

Magistrate aliuliza, unaweza kupata dhamana?" Ferreira alijibu kuwa wangetoa 16,000 fedha za Kireno alizokuwa nazo rafiki yake Joao, na thamani yake ikajulikana kuwa ni pauni 225 na kamera.

Juu ya swali ikiwa walikuwa na marafiki ambao wangejitoa kuaweke dhamana, Ferreira alimtaja Mayanja Masinde, mwananchi mkimbizi wa Mozambiki aliye Dar es Salaam.

Lakini Magistrate alisema kuwa haifai kukuwali dhamana ya mtu asiye na makao maalum.

"Kama nilivyo waelezeni" alisema Bw. Hakimu, "kortii hii haijapendezwa na kuingia kwenu katika nchi hii kwa njia mliyotumia. Kwa hiyo mtafikiwaki kisheria na kortii hii. Kuwa kinyume na utawala wa Dr. Salazar na chama chake si sababu ya kuingia Tanganyika.

Tukae pamoja

"Kwa kufuata maneno ya Mwongoza Mashstaka, na mapendekezo ya Serkali ya watu, kortii hii imeona lazima likubaliane haye, kortii litafuata mapendekezo ya watu na Serkali. Ingekuwa sawa na si haki kutoa dhamana katika kesi kama hii inayohusu usalama kwa hiyo natahirisha hadi tarehe 25 April, na washtakiwa watarudi rumande." (6)

Ferreira alirudia tena kusema, "naomba tukae wawili pamoja katika rumande," walakini Hakimu alimjibu, "Halikadhalika hili si shauri langu". Halafu Ferreira alitomba msamaha kwa yote aliyoyasema mbele ya kortii.